

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129

Nukushi: 026 -2322126

Baruapepe: km@michezo.go.tz

Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali- Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

***Dodoma,
22 Machi, 2024.***

TAARIFA KWA UMMA

MAADHIMISHO YA SIKU YA UKOMBOZI WA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA TAREHE 23 MACHI, 2024

Tarehe 23 Machi, 2024 Tanzania itaungana na Mataifa mengine ya Afrika kuadhimisha Siku ya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika kama juhudi za kuenzi na kuhifadhi historia ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Siku hiyo muhimu ilichaguliwa kama siku ya maadhimisho kutokana na tukio muhimu la mwaka 1988 ambapo majeshi ya Afrika yalihitimisha utawala wa kimabavu na ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini katika mji wa Cuito Cuanavale uliopo kusini mwa Angola. Tukio hilo lilipelekea utawala wa ubaguzi wa rangi na washirika wao kukubali kuzingatia Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSCR) 435/78, lililowezesha uhuru wa Namibia.

Aidha, mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Jijini Windhoek, Namibia Agosti, 2018 uliidhinisha tarehe 23 Machi ya kila mwaka kuwa ni siku ya kusherehekea ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika kama njia ya kuenzi na kuhifadhi historia ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Maadhimisho ya mwaka huu ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa ilitoa mchango mkubwa katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika chini ya uongozi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo Tanzania ilisimama kidete kusaidia vyama vya Ukombozi, mapambano yenyewe hadi uhuru na utawala wa haki ukapatikana kikamilifu. Pia, Tanzania ilichangia kwa hali na mali kwa kutumia rasilimali zake, nguvu za kidiplomasia na za kijeshi katika kusaidia mapambano hayo.

Kwa mwaka huu, Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Afrika yatafanyika kwenye Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kilichopo mtaa wa Garden Avenue, Jijini Dar es Salaam. Kituo hicho ndipo yalipokuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya OAU. Shughuli zitakazofanyika katika siku hiyo ni pamoja na Mdahalo kuhusu mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika na fursa za Urithi wa ukombozi katika nyanja za siasa, uchumi na jamii.

Mdahalo huo utaongozwa na nguli wa historia ya Ukombozi na mashuhuda wa harakati za Ukombozi, maonesho ya picha, kusikiliza hotuba za viongozi wa harakati za ukombozi na maonesho ya Makala jongefu kuhusu historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika. Shughuli zote zitaanza Saa nne asubuhi hadi Saa nane mchana na zitarushwa Mbashara kupitia kituo cha TBC na Chanel Ten.

Imetolewa na;-



Aron Msigwa

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI